# HADITHI AROBAINI
# ZA
# MTUME MUHAMMAD
# s.a.w.

## NENO LA MBELE

Hadithi hizi arobani zilizopigwa chapa katika kijitabu hiki, zililichaguliwa katika hadithi ndefu za Mtume s.a.w ... na Hazrat Mir Hohamed Ismail (Mungu amwie radhi) aliyekuwa Mtawa maarufu na walii Mtakatifu na mfuasi mwaminifu wa Seyidna Ahmad, Mjumbe wa Mungu wa siku hizi. Wasomaji watakapozisoma hadithi hizi zenye manufaa wamwombee yeye baraka nyingi pamoja na kumsalia Mtume s.a.w., kwa kumshukuru yeye juu ya ihsani aliyotufanyia kwa kutuongoza kwenye wema.


| | | |
|---|---|---|
| Chapa ya mara ya kwanza | 1956; | Nakili 3,000 |
| Chapa ya mara ya Pili | 1959; | Nakili 3,000 |
| Chapa ya mara ya Tatu | 1966; | Nakili 5,000 |
| Chapa ya mara ya Nne | 1971; | Nakili 5,000 |
| Chapa ya mara ya Tano | 1989, | Nakili 2,000 |
| Chapa ya mara ya Sita | 1996; | Nakili 5,000 |
| Chapa ya mara ya Saba | 2009; | Nakili 2,500 |

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْم

# DIBAJI

Mtume Muhammad s.a.w. alisema, “Mtu ye yote atakayekumbuka hadithi zangu arobaini kwa kuwafundisha dini umati wangu, Mwenyezi Mungu atamfufua siku ya Kiyama pamoja na mafukahaa, nami nitamwombea na kumshuhudia.” Kwa mujibu wa hadithi hii tulitangaza tafsiri na maelezo ya hadithi arobaini katika gazeti letu: “Mapenzi ya Mungu” tangu mwezi wa Septemba 1953, hadi mwezi wa June 1954. Wasomaji wetu walinufaika sana na walitaka hadithi hizo zichapishwe kwa sura ya kijitabu.

Leo kwa rehema za Mwenyezi Mungu, tumeweza kuzipigisha chapa kwa namna ya kijitabu na twawaomba ndugu zetu Waislamu wazisome kwa nia safi na mwili safi huku wakimsalia Mtume Mtukufu Bwana wetu Muhammad s.a.w. kwa kulipa ile ihsani aliyotufanyia kwa kutueleza mambo ya hekima kubwa ambayo yangetufaidisha katika maisha ya duniani na Akhera pia.

Hadithi zote za Mtume s.a.w., kwa hakika ni maelezo ya aya za Kurani Tukufu na zinatufunulia maana zake za ndani. Ndiyo sababu zimejaa hekima na maarifa na kila Mwislamu anatakiwa kuzielewa.

Yafaa sana kila hadithi isiyo kinyume cha Kurani Tukufu ishikwe na Waislamu na kitendo chao cho chote, kiwe hafifu namna gani, kisiachane na maagizo ya Mtume s.a.w.

Masahaba wa Mtume (Mungu awawie radhi) waliokuwa wasikilizaji wa kwanza wa maneno haya matakatifu na wenye kuyashika kwa shauku nyingi waling'aa kama nyota duniani. Sio kwamba waliinuka katika mambo ya dini peke yake bali hata katika elimu na siasa na mambo mengine walipita mataifa yote. Ndivyo zilivyo kubwa baraka za kumfuata Mtume s.a.w. Basi jamani, sisi pia natufanye hima kuyashika maagizo haya muhimu ili tuondokewe na uvivu, unyonge na umaskini na tuwe kama masahaba na Waislamu wa kwanza.

Tumechagua hadithi zilizo fupi ili kwamba watoto wadogo nao wasione shida kuzikumbuka na kufahamu maana yake.

Na maneno yetu ya mwisho ni kwamba sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Mlezi wa walimwengu wote.

**Sheikh Muhammad Munawwar.**

**Mubashir wa Islam**

**Masjid-el-Ahmadiyya. Nairobi,**

**12 Rabi-us-Sani, 1375 Hijriyyah, 28th Novemba, 1955.**

## اَلدِّينُ النَّصِيحَةُ

### 1. ADDIYNUN-NASIIHATU

**Dini ni nasaha**

Yaani ni nasaha kwa viumbe au kwa Mtume au kwa Mwenyezi Mungu. Ndiyo kusema kuwahurumia viumbe, kuishika dini ya Mwenyezi Mungu kwa uaminifu na kumsaidia Mtume katika kazi alizokabidhiwa na Mwenyezi Mungu.

## اِجْتَنِبُوا الْغَضَبَ

### 2. IJTANIBUL GHADHWABA

**Jiepusheni na hasira**

Mara nyingi hasira inaleta matusi, magomvi na hata kuuana.

## اَدُّوْا زَكٰوتَكُمْ

### 3. ADDUU ZAKAATAKUM

**Toeni zaka zenu**

Maana zaka ni msaada kwa mafukara na maskini na pia inatakasa mali ya mtu anayeitoa.

## اِحْفَظْ لِسَانَكَ

### 4. IHFADH LISAANAKA

**Linda ulimi wako**

Yaani usiwe na masingizio, uongo, utesi na maneno ya magomvi, machafuko, na maneno ya upuuzi.

## اَرْحَامُكُمْ اَرْحَامُكُمْ

### 5. ARHAAMUKUM ARHAAMUKUM

**Ndugu zenu ndio ndugn zenu**

Kwa hiyo wahurumieni, watendeeni mema, na wasaidieni zaidi kuliko wengine maana mmechangia damu.

## اَرْشِدُوْا اَخَاكُمْ

### 6. ARSHIDUU AKHAAKUM

**Waongozeni ndugu zenu**

Kwa kuwafundisha na kuwapa mawaidha na kuwakataza maovu ili wawe watu wema.

## اَسْلِمْ تَسْلَمْ

### 7. ASLIM TASLAM

**Silimu utasalimika**

Mwenye kuishika dini ya Kiislamu huepukana na kila namna ya upotevu uangamizao. Mwili wake, vitendo vyake na kikao chake husalimika na mambo yanayomletea maafa na aibu.

اَطِعْ اَبَاكَ

**8. ATWI’ ABAAKA**

**Watii wazazi wako**

Maana wametufanyia hisani kubwa kwa kutulea na kutusaidia na kututakia kila jambo la kheri. Basi ni wajibu wetu kulipa hisani yao kwa kuwastahi na kuwatii na kuwatendea kwa upole na adabu nyingi.

اِعْتَكِفْ وَصُمْ

**9. I’TAKIF WA SUM**

**Kaa katika i’tikafu na funga saumu**

Mwislamu anaposhinda msikitini siku tisa au kumi za mwisho za Ramadhani anapaswa kufunga saumu vile vile. Lau kama ashikwe na maradhi na kuacha saumu basi atoke msikitini pia, maana i’tikafu haiwi pasipo saumu.

اَعْلِنُوا النِّكَاحَ

**10. A’LINU NNIKAAHA**

**Itangazeni ndoa**

Kuoana kusiwe kwa siri. Amri hii imejaa hekima, Ndoa isiyotangazwa hadhara ya watu si halali.

اَكْرِمِ الشَّعْرَ

**11. AKRIM-I-SHSHA’RA**

**Ziheshimu nywele**

Imewekwa kanuni nzuri ya kuwaheshimu wazee ambao

wamekwisha kula chumvi nyingi. Wanastahiki kuheshimiwa na wadogo wao. Pia maana yake ni kwamba mtu ambapo huwa amekuza nywele inamlazimu aziangalie vizuri, zisiachwe tu kama washenzi.

اَلْاَيْمَنُ فَالْاَيْمَنُ

**12. AL-AIMANU FAL AIMANU**

**Wa kulia tena wa kulia wake**

Inapendeza kufanya kazi zote njema kwa mkono wa kulia. Watu wakikaribishwa vyakula, wa kulia apewe kwanza tena wa kulia wake na kadhalika. Na walapo wao wautumie mkono wa kuume.

اِشْفَعُوْا تُوْجَرُوْا

**13. ISHFA'UU TU'JARUU**

**Ombeeni, Mtapata ujira**

Tukiona mtu ananyimwa haki yake tusikawie kumwombea kwa wakuu wake. Naam, uombezi katika dhuluma na ujeuri hauna kheri kwa yo yote.

اَلْاَعْمَالُ بِالْخَوَاتِيْمِ

**14. AL-A'MAALU BILKHAWAATIIMI**

**Matendo hupimwa kwa mwisho wake**

Yaani mtu akiendelea na matendo mema mpaka kufa kwake atahesabika kuwa mwema, na matendo hayo yakikatika yakawa maovu baadaye akafa hali yu mwovu, basi atatendewa kama mtu aliyepotea njia. Tunaonywa tusijivunie mema tuliyoyafanya wala

tusikate tamaa tukiisha tenda maovu kwa bahati mbaya, maana twaweza kujisahihisha na kuachilia mbali yamchukizayo Mungu.

اُوْصِيْكُمْ بِالْجَارِ

**15. UUSWIIKUM BIL JAARI**

**Nawausieni juu ya jirani**

Dini ya Kiislamu imetia mkazo juu ya kuwatendea wema majirani. Jirani na awe mtu namna gani anastahiki kuangaliwa vizuri. Kuoneana huruma hukuza mapenzi na amani.

اَكْرِمُوْااَوْلَادَكُمْ

**16. AKRIMU AULAADAKUM**

**Waheshimuni watoto wenu**

Mtoto wa leo ni baba wa kesho. Lazima tuwafunze kujiheshimu na hivyo watakuwa na moyo wa kujitoa katika yale yanayowaletea aibu na pia watashika adabu njema ya kuwaheshimu wengine, wakubwa kwa wadogo. Kuwatolea ukali kila mara si vizuri.

اَلْاَمَانَةُ عِزٌّ

**17. AL-AMAANATU ‘IZZUN**

**Kuaminiwa ni heshima**

Yafaa Mwislamu akae duniani kwa jinsi itakayompelekea kuaminika. Mtume s.a.w. alipewa lakabu ya ‘Alamin’ (mwaminifu) na watu wake tangu alipokuwa kijana kwa sababu ya maisha yake yaliyotukuka. Mhaini hana heshima.

## بَجِّلُوا الْمَشَائِخَ

**18. BAJJILU-L-MASHAAIKHA**

**Waheshimuni wazee**

Kwani wameona ambayo sisi hatukuyaona. Elimu na maarifa waliyo nayo yatatufaidisha katika maisha yetu, na kwa kuwadharau tutajinyima kheri nyingi.

## تَعَلَّمُوا الْيَقِيْنَ

**19. TA'ALLAMUL-YAKIINA**

**Jifunzeni yakini**

Yakini maana yake ni kujua jambo fulani kwa hakika kuwa ndivyo. Yakini ndiyo msingi wa matendo yote. Mtu mwenye yakini kuwa mbegu zikipandikizwa zitaota ndiye anayeweza kuzitoa ghalani na kuzifukia ardhini. Watu ambao imani yao inalewalewa hawafiki mahali.

## تَهَادُوْا تَحَآبُّوْا

**20. TAHAADUU TAHAABBUU**

**Pelekeaneni zawadi mpendane**

Kupelekeana hedaya kunazidisha mapenzi. Mtu hali riziki ya mwigine lakini ni njia bora ya kuunga watu pamoja. Kurani Tukufu yasema, Mwislamu akiletewa zawadi na arudishe bora kuliko ile au sawa na aliyopewa.

## اَلتَّعْزِيَةُ مَرَّةً

**21. ATTA'ZIYATU MARRATAN**

**Kupeleka rambirambi kuwe mara moja tu**

Ni desturi mbaya kukusanyika mahali pa matanga na kukaa hapo hapo siku nyingi kuwatia gharama waliofiwa. Mtu aliyepatwa na

msiba lazima apewe mkono wa tanzia maana atafarijika lakini kuiendeleza muda mrefu kutamwongezea huzuni na mzigo.

اَلْخَالَةُ وَالِدَةٌ

**22. AL-KHAALATU WAALIDATUN**

**Dada ya mama ni mama**

Mtu amheshimu dada ya mama yake kama mama mzazi.
Na pia mtu akifiwa na mkewe akahitaji kuoa tena yafaa mchumba wake awe dada ya mkewe marehemu maana ataweza kutunza watoto wake na nyumba yake kama dada yake.

اَلدُّعَاءُ هُوَالْعِبَادَةُ

**23. ADDU'AAU HUWAL'IBAADATU**

**Maombi ndiyo ibada**

Mwislamu ambaye anamaliza sala yake upesi upesi bila ya kuomba mahitaji yake kwa Mwenyezi Mungu sala yake haina maana.

اَلدُّنْيَا مَزْرَعَةُ الْاٰخِرَةِ

**24. ADDUNYA MAZRA'ATUL - AAKHERATI**

**Dunia ndivo konde la Akhera**

Kila mtu ni mlimaji na cho chote atakachotenda katika
maisha ya dunia mfano wake ni kama mbegu ipandwayo kondeni na yeye atakwenda kuvuna matunda yake baada ya kufa kwake. Basi na aangalie apandacho.

صُوْمُوْا تَصِحُّوْا

**25. SUUMUU TASWIHHUU**

**Fungeni saumu mtapata afya**

Kama mtu afanyaye kazi siku zote bila kulala au kupumzika

huzeeka upesi hivyo tumbo la mtu likishurutishwa kufanya kazi yake daima halina hudi kuchoka upesi na kudhoofika. Basi kula shibe siku zote kunadhuru afya na tumbo halipati nafasi ya kupumzika. Zaidi ya chakula tukitumiacho hakibadiliki kifae mwilini bali kinapita tu pasipo kufaa cho chote. Kikitumiwa kiasi kinaleta afya na kujenga mwili. Mojawapo katika faida za saumu ni kutupatia uzima wa miili yetu.

اَلْعَيْنُ حَقٌّ

**26. AL'AINU HAQQUN**
**Kijicho ni haki**

الصَّبْرُ رِضًا

**27. AS-SABRU RIDHAN**
**Subira ni ridhaa**

Subira siyo kuvumilia taabu na hali mna mnung'uniko moyoni. Bali hakika ya subira, kama alivyosema Mtume, ni kuridhika na tendo la Mwenyezi Mungu liwe la kutupendeza au kutuchukiza.

اَلْمُحْتَكِرُ مَلْعُوْنٌ

**28. AL-MUHTAKIRU MAL'UUNUN**
**Azuiaye bidhaa anapatwa na mashaka**

Islamu inaruhusu biashara ya kawaida lakini inakataza tamaa ya kupata mali kwa njia isiyo halali. Watu wengi siku hizi hawataki kuwauzia wenzao bidhaa ili wapate kupandisha bei na kuchuma mali nyingi. Ijapo bidhaa inajaa ghalani lakini inazuiwa kuighalisha na kutaabisha wanunuzi. Hiyo inaleta taabu kwa kila mtu. Watu wasipopata mahitaji yao kwa bei ya kawaida huchukiwa sana na matendo ya wachuuzi na udanganyifu, wizi,

unyang'anyi na kutoaminiana huonekana katika nchi. Pengine vitu huchomwa moto. Matukio hayo yaleta dhara kwa wenye biashara na kwa serikali na wenyeji pia. Watu hao wataadhibiwa na Mwenyezi Mungu kwa sababu ya choyo na ubahili.

اَلْمُسْلِمُ اَخُوالْمُسْلِمِ

**29. AL-MUSLIM AKHUL-MUSLIM**

**Mwislamu ni ndugu wa Mwislamu**

Udugu wa dini huunganisha watu kama uungavyo ujamaa wa damu. Tunaweza kusema ya kuwa wenye imani kamili wanakuwa tayari kuachana na jamaa zao kwa ajili ya dini. Basi Waislamu tusighafilike na wajibu wetu wa kuwatumikia ndugu zetu Waislamu kwa njia yo yote iwezekanavyo. Udugu huu ukilegea Waislamu watatengana nayo ndiyo alama ya kupungua imani.

اَلْمَطْعُوْنُ شَهِيْدٌ

**30. AL-MAT'UUNU SHAAHIDUN**

**Mwenye kufa na tauni ni shahidi**

Tauni ni ugonjwa mbaya sana ambao unampa mtu udhia mkubwa mno. Mwislamu anayeugua ugonjwa huu ameitwa shahidi kwa sababu hupata taabu nyingi duniani. Na Mungu Mwenye huruma hataki kumwadhibu mara ya pili katika Akhera.

لَا وَصِيَّةَ لِوَارِثٍ

**31. LAA WASIYYATA LI WAARITHIN**

**Hapana wasia kwa warithi**

Sheria ya Islam imeweka sehemu maalumu kwa ajili ya jamaa fulani ya karibu katika mali yanayoachwa na maiti. Mathalan, mke katika hali moja anapokea sehemu ya nne (1/4) ya urithi wa mumewe marehemu na katika hali nyingine apata sehemu ya nane

(1/8). Hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu na mumewe hana haki ya kumwongezea kitu cho chote. Naam, anaweza kufanya wasia wa thuluthi ya mali yake kumpa rafiki zake au jamaa zake wasio na sehemu maalumu katika urithi au mayatima au kwa ajili ya dini. Kwa njia hii M wenyezi Mungu amezuia mtu ye yote asipokee mali nyingi peke yake. Watu wengi wakipata mali kidogo ni bora zaidi kuliko mtu mmoja kupata mali yote. Ndiyo njia ya amani, raha, na starehe.

لَا تَعُدْ فِي صَدَقَتِكَ

**32. LAA TA'UD FII SADAKATIKA**

**Usirejeshe sadaka yako**

Ukiisha kutoa chochote kuwa sadaka haipendezi kutamani kuichukua tena. Hata Mtume s.a.w. alikataza kukinunua kilichotolewa sadaka, maana alihofia pengine aliyepewa sadaka atapunjwa. Mwislamu hawi mchoyo.

اَلنَّدَمُ تَوْبَةٌ

**33. ANNADAMU TAUBATUN**

**Majuto ndiyo Toba**

Katika maneno haya mawili Mtume ameeleza hakika ya toba ni nini. Mkosaji apatwapo na majuto juu ya kitendo chake na anaazimu kwamba hatotenda maovu tena hupokewa kwenye baraza ya Mungu mwenye huruma. Rehema ya Mwenyezi Mungu inamfikia kila anayesikitikia matendo yake mabaya na yu tayari kuyaachilia mbali.

اِجْتَنِبُوْا كُلَّ مُسْكِرٍ

**34. IJTANIBUU KULA MUSKIRIN**

**Jiepusheni na kila kilevyacho**

Sheria ya Islam ndiyo ya kwanza kukataza vileo. Pombe za kila

aina, bangi, kasumba na namna nyingine yo yote ya kileo, kidogo au kingi, kimeharimishwa. Hasara ya mali na madhara ya vileo kwa mwili na akili ya binadamu vimethibitika siku hizi.

لَا تَتَمَنَّوُ االْمَوْتَ

## 35. LAA TATAMANNAWUL-MAUTA

**Msiitamani mauti**

Watu wengi wanapochukiwa na jambo fulani wanajiua. Hilo ni ujinga wa mwisho. Islamu inamfunza mtu asikate tamaa katika hali zote na afululize bidii na jitihada. Mwislamu ameumbwa kushinda na kutawala yote yaliyo kinyume chake. Anayeshindwa na kukata tamaa hawezi kuwa Mwislamu. Mtume s.a.w. alikataza kumsalia mtu aliyejinyonga, maana hakutegemea fadhili za Mwenyezi Mungu. Wanywaji wa pombe, kwa kawaida, huwa wepesi wa hasira na wanataka kujiokoa na maumivu kwa kujinyonga.

اَلسَّلاَمُ قَبْلَ الْكَلاَمِ

## 36. ASSALAAMU QABLAL KALAAM

**Maamkiano yawe kabla ya mazungumzo**

Ni adabu njema kumsalimu mtu kabla ya kusema naye maneno yo yote.

تَرْكُ الدُّعَاءِ مَعْصِيَةٌ

## 37. TARKUD-DUA'AAI MA'SIYATU

**Kuacha kuomba ni dhambi**

Maombi ndiyo sehemu kubwa ya ibada ya mwanadamu. Hata mtu akifanya kila tendo la heri kama kuwasaidia wenzake na kuhurumia kiumbe cha Mungu na kutazama wagonjwa na kutumikia maskini na wenye haja lakini anaacha kumuomba Mwenyezi Mungu bila shaka amepungua wema, bali ni mwenye

dhambi, maana tumeamuriwa kuomba na asiyedumisha maombi amevunja amri. Maombi hutuvutia baraka na rehema za Mwenyezi Mungu na hutuondolea mabalaa mengi yanayotaka kutuangamiza.

زِنْ وَارْجِحْ

**38. ZIN WA ARJIH**

**Pima na uongeze**

Kumpa mtu haki yake ni uadilifu, na kumwongezea ndiyo ihsani. Mtume s.a.w. ataka watu wapendane kwa kutendeana wema wao kwa wao. Wafanya biashara wamehusika sana na amri hii. Kumnyang'anya mtu haki yake ni mbali kabisa na mafunzo ya Islam.

اِتَّقُوااللّٰهَ فِى النِّسَآءِ

**39. ITTAQULLAAHA FIN-NISAAI**

**Mwogopeni Mwenyezi Mungu juu ya wanawake**

Maana wao ndio viumbe dhaifu wasioweza kulinda haki zao wenyewe. Basi wanaume wanaonywa wasiruke mipaka kwa kutojali haki zao. Ingawa dunia inaonekana kama imeendelea sana siku hizi lakini wanawake mpaka sasa wananyimwa haki zao.

طَلَبُ الحَلَالِ جِهَادٌ

**40. TALABUL-HALAALI JIHAADUN**

**Kutafuta riziki ya halali ni jihadi**

Uislamu unatufundisha kushika njia ya halali katika mambo yote. Siku hizi unyang'anyi na udanganyifu vimetapakaa kila mahali na imekuwa rahisi sana kupata mali kwa njia zilizokatazwa na sheria ya Mwenyezi Mungu. Basi huwa shida kabisa kupata riziki ya halali na mtu asipoangalia sana mara huangukia haramu na mali iliyo najisi. Inatakiwa juhudi kubwa na uangalifu mwingi katika kupambanua kati ya haramu na halali. Kwa ajili hii Mtume s.a.w. alisema kwamba mwenye kutafuta riziki ya halali atapata thawabu kama yule aliyepigana vita katika njia ya Mwenyezi Mungu.